- ***Mhe. George Boniface Simbachawene (MB), Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora,***
- ***Mhe. Deus Clement Sangu (Mb); Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;***
- ***Mhe. Rosemary Senyamule, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma;***
- ***Bw. Juma Selemani Mkomi, Katibu Mkuu,Ofisi ya Rais,Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;***
- ***Wahe. Wakuu wa Wilaya za Mkoa wa Dodoma;***
- ***Bw. Xavier Daudi, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;***
- ***Bw. Abdul- Razaq Badru, Mwenyekiti wa Bodi - Watumishi Housing Investments (WHI) na Wajumbe wote wa Bodi;***
- ***Dkt. Fred Msemwa, Mkurugenzi Mkuu & Wafanyakazi wote wa Watumishi Housing Investments;***
- ***Waandishi wa Habari;***
- ***Mabibi na Mabwana.***

Ni furaha kubwa kushiriki pamoja nanyi katika uzinduzi wa Mpango wa Makazi kwa watumishi wa umma ambao ni muhimu katika ustawi wa watumishi. Nakushukuru sana Mhe. George Simbachawene, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kunipa fursa ya kuwa sehemu ya historia ya Mpango huu adhimu. Pia, nawashukuru na kuwapongeza nyote mliofanikisha Mpango huu na pia hafla hii ya uzinduzi.

**Waheshimiwa Viongozi na Washiriki wote;**

Ibara ya 9D ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2020 – 2025) inaelekeza Serikali kuwa upatikanaji wa huduma ya makazi iwe kipaumbele ihamasishe na kuweka mazingira wezeshi ili wananchi katika maeneo yote nchini wawe na makazi bora. Nimefahamishwa kuwa katika kipindi cha miaka kumi iliyopita, *Watumishi Housing Investments,* kupitia Mpango wa Makazi kwa Watumishi wa Umma, imefanikiwa kujenga nyumba 1,006, katika mikoa 19 nchini. Hadi sasa, sehemu kubwa ya nyumba hizo zimekwishauzwa kwa watumishi wa umma.

Hata hivyo, ili Mpango huu uweze kufikia ufanisi wa hali ya juu, ni muhimu kuweka taratibu rafiki zinazowawezesha watumishi wa umma na wanachama wa mifuko ya hifadhi ya jamii, kumudu kununua nyumba kwa kutumia mishahara yao. Hivyo, ninapongeza sana hatua zilizochukuliwa na *Watumishi Housing Investments* katika kuwezesha malipo ya ununuzi wa nyumba kwa njia rafiki, kama kulipia nyumba taratibu taratibu ikiwa inaendelea kujengwa, au malipo ya nyumba wakati mtumishi akiendelea kuishi ndani ya nyumba hiyo kupitia malipo ya kila mwezi. Ninapongeza pia utolewaji wa hatimiliki kwa wanunuzi wa nyumba, kwani ni hatua nzuri ya kuwawezesha kiuchumi Watumishi wa Umma, endapo zitatumika kuomba mikopo ili kupata mitaji.

**Waheshimiwa Viongozi na Washiriki wote;**

Mpango huu unalenga kupunguza changamoto za makazi kwa watumishi wa umma, hususan wa walimu, madaktari, wauguzi, na watendaji wa Serikali, kwa kutoa makazi

bora na kwa gharama nafuu. Mbali na kupunguza uhaba wa makazi, pia ni kichocheo cha ukuaji wa uchumi kwa kutoa ajira na kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya ujenzi, hususan wa makazi. Serikali inaamini kwamba nyumba hizi zitakuwa suluhisho la muda mrefu kwa changamoto ya uhaba wa makazi nchini, na hivyo kuboresha ustawi wa jamii kwa ujumla. Kwa kuzingatia umuhimu wa makazi bora kwa watumishi wa umma, Mpango wa Makazi kwa Watumishi ni hatua muhimu katika kuboresha utendaji wao kazini kwa kutoa huduma bora na kuhakikisha ustawi wa maisha yao. Napenda kuwahakikishia kuwa, Serikali ya awamu ya sita itaendelea kushirikiana na mifuko ya hifadhi ya jamii na sekta binafsi ili kuhakikisha rasilimali zinazohitajika katika kutekeleza miradi hii zinapatikana kwa wakati na kwa njia endelevu.

**Waheshimiwa Viongozi na Washiriki wote;**
Ili mpango huu uweze kufikia malengo yake, ni muhimu pia kuhakikisha uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wake kwa kuwashirikisha wadau. Mpango huu unawezesha upatikanaji wa makazi bora kwa watumishi wake, na kuhakikisha watumishi wenye uhitaji wa makazi wanapata fursa ya kumiliki nyumba bora. Aidha, ni imani yangu kuwa ujenzi wa nyumba za watumishi wilayani na vijijini, utachochea maendeleo katika maeneo hayo. Hivyo, napenda kutoa rai kwa wadau mbalimbali hususan sekta binafsi, kuunga mkono jitihada hizi ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa mpango huu na hivyo kufikia malengo yaliyokusudiwa.

**Waheshimiwa Viongozi na Washiriki wote;**
Serikali imedhamiria kuona miradi kama hii inatekelezwa katika mikoa na wilaya zote nchini, ili kuhakikisha kuwa sehemu kubwa ya Watumishi wa Umma wanaishi katika nyumba bora, na hivyo kuwawezesha kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi. Aidha, nimefurahishwa na kuanzishwa kwa Mfuko wa Uwekezaji wa Pamoja wa *Faida Fund*, ambao unalenga kuwawezesha watumishi wa umma, na wananchi kwa ujumla, kumudu gharama za nyumba kwa ajili ya makazi. Ninawahimiza watumishi wa umma na wananchi wote kuchangamkia fursa ya uwekezaji katika Mfuko huu ili kufikia ndoto zao za kumiliki nyumba bora. Aidha, hatua ya *Watumishi Housing Investments* ya kupunguza bei za nyumba kwa kati ya 10% na 30%, ikilinganishwa na bei za soko, ni ya kupongezwa kwa sababu hatua hiyo inawawezesha watumishi wa umma na wananchi kwa ujumla kumudu gharama za nyumba hizi. Pia, natoa rai kwa *Watumishi Housing Investments* kuimarisha na kuendeleza ushirikiano uliopo na Mabenki mbalimbali ambao unawezesha kupatikana kwa mikopo ya nyumba yenye riba nafuu, ambayo imesaidia sana watumishi wa umma kuweza kununua nyumba. Serikali itaendelea kuunga mkono jitihada hizi ili kufikia lengo la kuwawezesha watumishi wa umma kupata makazi bora.

**Waheshimiwa Viongozi na Washiriki wote;**
Ili kukabiliana na uhaba wa makazi kwa watumishi kupitia utekelezaji wa Mpango wa makazi bora kwa watumishi wa umma, napenda kutumia hafla hii kusisitiza masuala muhimu, kama ifuatavyo:

**Kwanza,** ninatambua changamoto kubwa ya upatikanaji wa viwanja vya kutosha katika maeneo mengi, hususan maeneo ya mijini. Hivyo, ili kuufanya Mpango huu kuwa endelevu, ninashauri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi na Halmashauri husika kufanyia kazi suala hili ili kuhakikisha upatikanaji wa maeneo ya ujenzi wa nyumba za watumishi yaliyo karibu zaidi na sehemu

za kazi, na yanayozingatia mahitaji ya msingi ya watumishi na familia zao, hivi sasa na kwa wakati ujao. Aidha, napenda kusisitiza kuwa nyumba zinazojengwa na *Watumishi Housing Investments*, lazima zizingatie ubora na viwango stahiki ili kuendana na thamani ya fedha na kuwaepushia wanunuzi wa nyumba hizo gharama za marekebisho na maboresho zaidi.

**Pili,** ili mpango huu uweze kufikia malengo yake na kuwa na manufaa kwa watumishi, ni muhimu vigezo na masharti ya upatikanaji wa nyumba kwa watumishi wa umma viheshimiwe na kuzingatiwa. Upokeaji, uchambuzi wa maombi na uthamini wa nyumba hizo vifanyike kwa haki na kuzingatia uhalisia. Aidha, juhudi za makusudi zifanyike ili watumishi wa ngazi za chini na kati wapewe kipaumbele katika upatikanaji wa nyumba hizo.

**Tatu,** natoa rai kwa watumishi na wananchi ambao watapata nafasi ya kununua nyumba hizi kuzitunza ili zibaki katika hali ya ubora kadri inavyowezekana. Matunzo ya nyumba hizi yajumuishe miundombinu na mazingira yanayozunguka eneo la nyumba. Ninawasihi kupanda miti na maua ili kuleta mandhari nzuri na pia kuhakikisha usafi muda wote. Angalieni pia uwezekano wa kushirikisha taasisi au watu binafsi wenye utaalam wa kupendezesha makazi *(landscaping).* Aidha, napenda kuwakumbusha *Watumishi Housing Investments* kupanda miti katika maeneo yote inakotekelezwa miradi ya ujenzi wa nyumba za makazi kwa watumishi wa umma ili kuhifadhi na kutunza mazingira. Vilevile, ujenzi wa nyumba za makazi ya watumishi uzingatie uwepo wa viwanja vya michezo, maeneo ya kupumzikia na huduma nyingine za jamii kama elimu, afya na huduma za mahitaji ya maisha, kama maduka na maeneo ya ukusanyaji wa taka. Hii ni kwa kuwa makazi haya yanaleta pamoja idadi kubwa ya watu, wenye mahitaji tofauti tofauti.

**Nne,** hospitali yetu ya Benjamin Mkapa ambayo iko jirani na hapa Njedengwa ina uhaba mkubwa wa nyumba za makazi kwa ajili ya madaktari na wauguzi. Ninawaomba *Watumishi Housing Investments* kutoa kipaumbele kwa watumishi wa hospitali hiyo katika uuzaji wa nyumba zitakazoendelea kujengwa hapa Dodoma ili waweze kutoa huduma kwa Watanzania wakiwa karibu na hospitali.

**Tano,** kwa kuwa mahitaji ya nyumba nchini bado ni makubwa, ninawaachia Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na *Watumishi Housing Investments* changamoto ya kutafuta vyanzo vingine ya fedha kwa ajili ya upanuzi wa mradi huu. Mbali ya fedha kutoka Serikalini, angalieni uwezekano wa kupanua vyanzo vya upatikanaji wa fedha kupitia Hatifungani, Makampuni ya Bima, Wadau wa Maendeleo, Taasisi za kifedha na Uwekezaji kutoka Taasisi nyingine na hata mtu mmoja mmoja.

**Mwisho**, naipongeza Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na *Watumishi Housing Investments* kwa kuja na mradi huu muhimu. Aidha, nawasihi watumishi wa umma kuchangamkia fursa hii adhimu, ya kujipatia makazi bora kupitia nyumba zinazojengwa na *Watumishi Housing Investments*.

Baada ya kusema haya, sasa nipo tayari kuzindua rasmi Mpango wa Makazi bora kwa Watumishi wa Umma ulioanza kutekelezwa hapa Njedengwa, Dodoma.

**Asanteni sana kwa kunisikiliza!**